

Unda seti yako ya mahitaji ya kukabiliana na kukatika kwa umeme wakati wa dhoruba



Kutegemea na hali ya hewa na sababu nyinginezo, wakati wa dhoruba umeme unaweza kukatika kwa saa au siku kadhaa. Unapaswa kuwa na akiba ya kutosha ili kukimu familia yako kwa angalau siku tatu. Tunapendekeza uweke vifaa kwenye vyombo visivyoingiza maji na visivyoruhusu panya kuingia na urudishie mahitaji kwenye kisanduku chako walau mara moja kwa mwaka.

- Kurunzi au tochi ya kuvaa kichwani
- Redio inayotumia betri au nishati inayotokana na kuzungusha mpini kwa mkono
- Saa ya ukutani au mkononi inayotumia betri
- Betri za ziada
- Simu za kiganjani na chaja, ikijumuisha chaja ya gari
- Maji, galoni moja kwa kila mtu kwa siku, hasa ikiwa unategemea pampu ya umeme ili kupata maji
- Chakula kisichoharibika na kifungua makopo, mabakuli, sufuria na vyombo
- Betri za ziada kwa ajili ya matangi ya oksijeni au vifaa vingine vya matibabu
- Michezo ya bodi, vitabu na karata
- Jiko la kuchomea, jiko la gas la kuchomea mishikaki au jiko linalotumika kambini kwa ajili ya matumizi ya nje, pia mafuta na viberiti

Vifaa vya kisanduku cha dharura ambavyo vinaweza kuwa na umuhimu

- Vitu vinavyohitajika wakati wa kuhama kama funguo, mkoba au pochi, miwani, kitambulisho, hati ya kusafiria, vyeti vya kuzaliwa, taarifa za bima, kumbukumbu za kifedha, na karatasi yenye ramani ya eneo lako
- Nakala ngumu za Mpango wa Dharura wa Familia yako na orodha ya mawasiliano
- Miwani, meno bandia, visaidizi vya kusikia n.k.
- Dawa za kuandikiwa na dawa za kununua dukani, vifaa tiba na vifaa kama oksijeni ya ziada
- Mahitaji ya mtoto mchanga, maziwa na/au chakula, nepi na karatasi za kusafishia
- Mahitaji ya wanyama vipenzi, mikanda yenye lebo za vitambulisho na kamba/kifaa cha kuwabebea, chakula na maji, vifaa vya kufanyia usafi (yaani takataka) na dawa
- Mahitaji kwa ajili ya usafi binafsi, karatasi za kupangusia, sabuni, shampuu, brashi/chanuo, dawa ya meno na miswaki, kiondoa harufu, mahitaji ya wanawake na mafuta ya kuzuia mionzi ya jua
- Kisanduku na kitabu cha huduma ya kwanza, viua vimelea, bandeji mnato, plasta, gundi mnato, bandeji, viungio, dawa ya kuoshea macho, dawa za mafua na dawa ya kutibu majeraha ya moto
- Nguo, viatu/mabuti, makoti mazito ya kuzuia baridi, glovu za kazi, ziada ya nguo za ndani na soksi
- Mito na mablanketi au mifuko ya kulalia
- Bidhaa za karatasi na vifaa vya usafi, sahani za karatasi, taalo za karatasi, karatasi za chooni na mifuko ya kuhifadhiya taka
- Barakoa za kuzuia vumbi au kufunika uso, miwani ya macho na glovu zilizoundwa kwa mpira
- Spana au koleo kwa ajili ya kuzima huduma na kisu au kifaa chenye matumizi mbalimbali
- Firimbi kwa ajili ya kuita msaada
- Gundi ya karatasi, kamba ngumu, karatasi na kalamu kwa ajili ya kuandika maandishi au kuweka lebo kwenye vifaa

Saidia betri ya kifaa chako iweze kudumu

- Usizime simu — kompyuta ubao au simu hutumia betri zaidi pale inapowashwa na kuzimwa, hivyo badala yake tumia hali tuli.
- Lemaza Bluetooth na arifa usizohitaji wewe mwenyewe (usizime arifa za dharura). Zima Wi-Fi ikiwa huna uhitaji nayo.
- Punguza mwanga wa onyesho uwe chini kwa kadri inavyowezekana.
- Funga programu ukimaliza kuzitumia.



Andaa mpango wa kukabiliana na ukosefu wa umeme kwa muda mrefu



- Jiandae kwa mahitaji ya kaya.
 - Kusanya vitu vinavyohitajika ili kuwaweka salama, mkila, na kustarehe.
- Jiandae kwa mahitaji ya wanyama vipenzi na mifugo.
 - Andaa mpango wa malisho na umwagiliaji iwapo pampu za kusukuma maji kutoka mtoni hazina nishati.
- Jiandae kwa mahitaji ya matibabu ili bado uweze kuendesha vifaa vya kitabibu hata kukiwa hakuna huduma ya umeme.
 - Jiandikishe katika mpango **Medical Certificate program (wetu wa Cheti cha Matibabu)** — hii hutujulisha palipo na mahitaji muhimu ili tuweze kuwasiliana nawe kwa uthabiti kuhusu kukatika kwa umeme.
- Panga mapema kuhamia kwa rafiki, au mwanafamilia au kwenye makazi ikiwa kutakuwa na ulazima, hasa kama una mahitaji ya matibabu ambayo yanahitaji umeme au ukiwa unafanya kazi au kusoma ukiwa nyumbani.
- Zingatia kununua jenereta ya cherezo na ufuatae maelekezo ya mtengenezaji ili kuitumia kwa usalama.
- Ikiwa una paneli za umeme wa jua, zingatia kuongeza **hifadhi ya betri**.

Jiandae kwa dharura

Pata maelezo zaidi kutoka **Msalaba Mwekundu** na **ready.gov** kuhusu jinsi ya kuweka familia na nyumba yako salama.

- Panga njia yako ya kuhama ikiwa kuna ulazima (tazama mwongozo wa kuhama wa nchi yako) na hakikisha gari lako lina mafuta.
- Kusanya nakala ngumu za vitu utakavyohitaji wakati wa kuhama, kama kitambulisho, kumbukumbu za kisheria, vyeti vya kuzaliwa na kadi za ruzuku ya serikali.

Jua unachomiliki

Piga picha ya kila chumba kilichopo kwenye nyumba yako, ikijumuisha karakana na kibanda chako, hivyo uwe na idadi ya vitu vyako ikiwa utahitaji kudai fidia ya bima. Fungua makabati ya vyombo na nguo pamoja na droo na upige picha kila kitu.

Rasilimali

- 211info.org
- publicalerts.org
- Madai Portland General Electric (PGE) portlandgeneral.com/claims
- ready.gov
- American Red Cross redcross.org/get-help

